




TAMICO

Uchaguzi Mkuu 2026

RUBARA



MARANDO

MANIFESTO YA UONGOZI

Mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti

Chama Imara, Mwanachama Salama. Pamoja Tunajenga!

SALAMU NA UTANGULIZI

Ndugu wanachama, viongozi wa matawi, wawakilishi wa makundi maalum na wajumbe wa Mkutano Mkuu, nawasalimu kwa jina la mshikamano wa wafanyakazi.

Nimejitokeza kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa chama chetu kwa sababu moja kuu: chama chetu kinastahili kuwa na nguvu zaidi, kuonekana zaidi, na kuleta matokeo yanayogusa maisha ya kila mwanachama — kazini na nyumbani.

Rubara Marando

Mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti

MIMI NI NANI

Naitwa Rubara Marando, mtumishi wa umma na mwanachama hai wa chama. Ninaleta uzoefu wa uongozi, usimamizi wa mikataba na uandaaji wa mipango wenye matokeo.

Cheo kazini

**Mhandisi Mkuu (Principal Engineer),
TANROADS Mkoa wa Ruvuma**

Taaluma

**Mhandisi Mtaalamu aliyesajiliwa na ERB (PE
4030); Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa
Ujenzi (MSc Construction Management)**

Uzoefu wa uongozi

**Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha
Mipango, TANROADS Geita na Ruvuma**

Lugha

Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha

NAFASI NILIZOSHIKA NDANI YA CHAMA

Mjumbe wa Tawi, Mkoa na Kanda 2016–2021

Mjumbe wa KUT-TAMICO 2016–2021

Mjumbe wa KUT-TUCTA 2016–2021

DIRA NA DHAMIRA

DIRA

Kuwa chama cha wafanyakazi kinachothamini nguvu ya majadiliano, na huduma bora kwa kila mwanachama.

DHAMIRA

Kutetea haki, maslahi na ustawi wa wanachama kupitia majadiliano yenye ushahidi, uongozi shirikishi, matumizi ya teknolojia, na uzingatiaji kamili wa Katiba na Kanuni za chama.

MISINGI YA UONGOZI WANGU

UWAZI

taarifa za utendaji kazi wa chama kwa kila robo.

USHIRIKISHWAJI

maamuzi kufanywa na vyombo vyenye dhamana katika ngazi husika.

UWAJIBIKAJI

ahadi zitapimwa kwa viashiria vinavyopimika.

UADILIFU

Katiba na Kanuni ndizo dira ya kila hatua.

MATOKEO

kipimo cha uongozi ni maisha bora ya mwanachama.

VIPAUMBELE VYANGU

Vipaumbele vyangu vimepangwa katika maeneo manne: Wanachama, Watumishi wa Chama, Kukua kwa Chama, na Utawala Bora.

A. WANACHAMA

1

Mikataba ya Hali Bora (CBA)

Kujadiliana na kusaini Mikataba ya Hali Bora (CBAs) katika kila taasisi yenye wanachama.

Kutoa mafunzo kwa watendaji na viongozi wa matawi ya masuala ya maslahi ya watumishi.

Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya Hali Bora (CBAs) iliyosainiwa, si kuisaini tu.

2

Bima za Afya na Motisha (Incentives) za Taasisi za Umma

Kujadiliana na waajiri kuweka ruzuku bima ya NHIF ili kupanua wigo wa huduma kwa watumishi.

Kudai motisha (Incentives) kwa watumishi ili kuongeza ari ya utendaji.

3

Msaada wa Kisheria

Dawati la msaada wa kisheria kwa migogoro ya kikazi, kufukuzwa kazi na makosa ya kinidhamu.

Kuwawakilisha wanachama katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Mahakama ya Kazi.

4

Elimu na Mafunzo

Mafunzo ya sheria za kazi, haki za mfanyakazi na majadiliano kwa viongozi wa matawi.

Kuhakikisha taasisi zinaandaa semina za maandalizi ya kustaafu na usimamizi wa fedha binafsi.

Kuandaa viongozi chipukizi kwa uongozi wa baadaye.

B. WATUMISHI WA CHAMA

5

Scheme of Service Bora kwa Watendaji

- Kuandaa na kuidhinisha Scheme of Service kwa watendaji wa chama.
- Maboresho ya mishahara na stahiki zinazoendana na gharama za maisha.
- Mafunzo endelevu na mazingira bora ya kazi.
- Tathmini ya utendaji iliyo wazi na motisha kwa wanaofanya vizuri.

C. KUKUA KWA CHAMA

6

Kuongeza Matawi, Idadi ya Wanachama, na Kuyalinda

- Nguvu ya chama ni idadi ya wanachama. Bila wingi hatuna sauti mezani.
- Kubaini maeneo mapya ya waajiri.
- Kampeni maalum ya usajili katika taasisi zisizo na matawi.
- Kufufua matawi yaliyolala na kuyapa mafunzo ya uongozi na nyenzo za kazi.

7

Ofisi za Makao Makuu ya Chama Dodoma

- Chama kinapaswa kuwa karibu na makao makuu ya Serikali.
- Kutumia ujuzi wa wanachama kuandaa nyaraka za ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu, Dodoma.
- Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu mwaka 2027.
- Jengo litajumuisha miradi ya kuingiza mapato.

8

Chama cha Kidigitali

- Kanzidata (database) ya wanachama yenye usajili mtandaoni na kadi za kidigitali.
- Uwasilishaji wa taarifa za utendaji kupitia mtandao.
- Usambazaji wa jarida (Newsletter) kwa wanachama kila robo mwaka.
- Utwaaji na uwasilishaji wa fomu za kugombea mtandaoni.

D. UTAWALA BORA

9

Kulinda Katiba na Kanuni za Chama

Kusimamia uzingatiaji kamili wa Katiba na Kanuni katika chaguzi, vikao na matumizi ya fedha.

Kuhakikisha vikao vya kikatiba vinafanyika kwa wakati na kumbukumbu zinatunzwa.

Kusambaza nakala za Katiba kwa kila tawi na kuwaelimisha wanachama haki zao.

Mapitio shirikishi ya Katiba pale inapohitajika, kwa ridhaa ya Mkutano Mkuu.

10

Kushirikisha Viongozi wa Makundi katika Maamuzi

Uwakilishi halisi wa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na kada mbalimbali katika vikao vya maamuzi.

Kuimarisha kamati za wanawake na vijana kwa bajeti na majukumu ya wazi.

11

Mfumo wa Maoni, Malalamiko na Maswali Wenye Majibu ya Wazi

Kila mwanachama ana haki ya kusikilizwa na kujibiwa. Hakuna hoja itakayopotea.

Kuwasilisha: mfumo wa mtandaoni (tovuti/app).

Namba ya ufuatiliaji: kila hoja inapata namba ya kumbukumbu ili mwanachama afuatilie hatua yake.

Muda wa kujibu: kukiri kupokea ndani ya siku 3; jibu kamili ndani ya siku 14.

Hali ya hoja inaonekana:

imepokelewa ▶ **inashughulikiwa** ▶ **imejibiwa** ▶ **imefungwa**

Maswali na Majibu: maswali yanayojirudia na majibu yake yanawekwa wazi kwa wanachama wote.

Usiri na ulinzi: hakuna mwanachama/mtendaji atakayeadhibiwa kwa kutoa maoni au lawama.

Ripoti ya wazi: idadi ya hoja zilizopokelewa na kujibiwa kutolewa kila robo mwaka.

12

Ushirikiano na Wadau

Kuimarisha uhusiano na Serikali, waajiri, TUCTA na washirika wa kimataifa.

Kushiriki kikamilifu katika Mabaraza ya Wafanyakazi ya taasisi.

100 SIKU ZA KWANZA

AHADI ZA SIKU 100 ZA KWANZA

- ✓ Kukutana na viongozi wa matawi yote na makundi maalum kusikiliza vipaumbele vyao.
- ✓ Kufanya tathmini ya hali ya fedha, mali na madeni ya chama, na kuitoa kwa wanachama.
- ✓ Kuorodhesha taasisi zisizo na matawi na kuzindua kampeni ya usajili.
- ✓ Kuorodhesha mikataba ya hali bora iliyopo, iliyokwisha muda na inayohitajika.
- ✓ Kuunda kamati ya mradi wa Makao Makuu Dodoma na kuanza mchakato wa ujenzi.
- ✓ Kuanza ujenzi wa kanzidata ya kidigitali ya wanachama.
- ✓ Kuzindua dawati la malalamiko na msaada wa kisheria.

JINSI MTAKAVYONIPIMA

Kila ahadi itakuwa na kiashiria kinachopimika na taarifa ya utekelezaji itawasilishwa kila mwaka mbele ya Mkutano Mkuu.

Eneo	Kiashiria cha mafanikio	Muda
Wanachama na matawi	Ongezeko la wanachama kwa 30% na matawi mapya katika taasisi zisizo na matawi	Miaka 2
Mikataba ya Hali Bora	Kila tawi kuwa na CBA hai iliyosainiwa	Miaka 3
Makao Makuu Dodoma	Kujengwa ofisi za makao makuu	Miaka 3
Scheme of Service	Scheme of Service ya watendaji kuidhinishwa na kuanza kutumika	Mwaka 1
Bima ya afya na motisha	Makubaliano mapya ya maboresho na waajiri	Miaka 2
Mifumo ya kidigitali	Wanachama wote kusajiliwa kwenye kanzidata; kadi za kidigitali	Mwaka 1
Katiba na Kanuni	Vikao vyote vya kikatiba kufanyika kwa wakati	Kila mwaka
Ushirikishwaji	Makundi maalum kuwakilishwa katika kila kikao cha maamuzi	Mwaka 1
Uwazi wa fedha	Taarifa za fedha kila robo mwaka; ukaguzi wa nje kila mwaka	Kila robo
Maoni, malalamiko na maswali	Mfumo kufanya kazi; angalau 90% ya hoja kujibiwa ndani ya siku 14	Miezi 6

HITIMISHO NA WITO WA KURA

Ndugu wanachama, chama hiki ni chetu sote. Hakijengwi na mtu mmoja, bali na wanachama wanaoshikamana chini ya uongozi wenye maono, uwazi na uwajibikaji.

Ninaomba ridhaa yenu tujenge pamoja chama chenye matawi imara, mikataba bora, makao makuu yetu wenyewe Dodoma, mifumo ya kisasa, na sauti ya kila kundi katika maamuzi.

NIPENI KURA ZENU ZA NDIO

Tulinde haki zetu, tuboreshe maslahi yetu, tujenge chama chetu.

**CHAMA IMARA, MWANACHAMA
SALAMA.
PAMOJA TUNAJENGA!**

Rubara Marando — Mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti

RUBARA MARANDO • UENYEKITI WA CHAMA



TAMICO

Uchaguzi Mkuu 2026

Tanzania Mines Energy Construction and Allied Workers Union